



**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb.Na.KGR/BMC/S.35/49/97

02/12/2022

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (TANGAZO LINARUDIWA)**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba anapenda kuwatangazia watazania wote wenye sifa kutuma maombi ya nafasi za kazi kama ifuatavyo:

### **1. MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II - NAFASI 2**

#### **A: SIFA ZA MWOMBAJI:**

- i) Aliyefaulu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)
- ii) Awe na Cheti cha Mafunzo ya Uhudumu wa Jikoni kutoka katika Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

#### **B: MAJUKUMU YA MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II**

- i) Kusafisha vyombo vya kupikia
- ii) Kusafisha vyombo vya kulia chakula
- iii) Kusafisha sehemu ya kulia chakula
- iv) Kuwatayarishia Wapishi/Waandazi vifaa vya kazi
- v) Kusafisha maeneo ya kupikia

#### **C: MSHAHARA**

Cheo cha Mhudumu wa Jikoni Daraja la II kina mshahara wa **TGOS A** kwa mwezi.

#### **MASHARTI YA JUMLA**

- i) Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania
- ii) Waombaji wote wawe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45

- iii) Waombaji wote wawe hawajawahi kupatikana na kosa la jinai, kugushi vyeti au kufungwa jela.
- iv) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminka pamoja na namba zao za simu.
- v) Waombaji wote waambatishe nakala za vyeti vya elimu, vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha 1 (passport size) ya hivi karibuni iliyoandikwa jina la mwombaji nyuma.
- vi) Waombaji wote waambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA
- vii) Testimonials "Transcripts", "Provisional Results", "Statement of results", na "Result Slips" hazitakubaliwa.
- viii) Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganifu na NECTA na NACTE
- ix) Mwisho wa kuleta maombi ni tarehe **08/12/2022 saa 9:30** mchana.
- x) Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa:-

**MKURUGENZI WA MANISPAA,  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA,  
S.L.P. 284,  
BUKOBA.**

  
Hamid A. Njovu  
**MKURUGENZI WA MANISPAA  
BUKOBA**

**MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
BUKOBA**

**Nakala: Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira,  
[www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz)**

**“ Tovuti ya Halmashauri ya Manispaa Bukoba,  
[www.bukobamc.go.tz](http://www.bukobamc.go.tz)**

**“ Mbao za Matangazo**